



Wewe na Mkalimani wako wa Mahakama
Kujilinda wakati wa COVID-19

Mahakama inakutaka wewe, mkalimani wako wa mahakama, na kila mtu aliye mahakamani kujilinda wakati wa dharura ya COVID-19.

Mkalimani wako ata:

- Atavalia barakoa (wkalimani wa lugha ya ishara hawahitajiki kuvaa barakoa)
- Kadri iwezekanavyo, adumishe umbali wa futi 6
- Atatafuta maeneo faragha ya kufasiri kwa ajili ya uwekaji mzuri wa umbali kati ya watu
- Atatumia vipokea sauti vya masikio au zana nyinginezo ili kufasiri kwa umbali ulio salama
- Kushirikiana na wafanyikazi wa mahakama ili kudumisha utakasaji wa vifaa
- Awe mwangalifu kuhusu kugusa makaratasi ambayo watu wengine wamegusa

Mkalimani wako HATA:

- Kusalimu kwa mkono
- Songea karibu nawe kwa ufasiri wa ufaragha zaidi
- Tumia kalamu au karatasi pamoja nawe
- Gusa simu yako ya mkononi/kifaa cha simu, hata kuangalia au kutafsiri ushahidi

Jinsi ya kujilinda ukiwa mahakamani:

YA KUFANYA:

- Nawa mikono yako mara kwa mara na sabuni na maji kwa angalau sekunde 20:
 - Baada ya kupenga kamasi, kukohoa, kupiga chafya, au kutumia maliwato; na
 - Kabla ya kula au kuandaa chakula cha kulisha mtoto

Usifanye HAYA:

- Kusalimiana kwa mkono, kugusa vitufe vya lifti, vishikio vya ngazi, au vitasa vya milango. Kutumia glavu au tishu kisha kutupa kiholela
- Ukigusa kitu chochote, usiguse uso wako - hasa macho, pua na mdomo wako - hadi utakapo nawa mikono yako
- Usiguse macho, pua na mdomo wako kwa mikono isiyosafishwa

Omba mahakama ipange upya tarehe yako ya mahakamani ikiwa:

- Una dalili au unapona kutokana na coronavirus, au
- Mtaalam wa afya alikuambia ujiweke katika karantini ya binafsi

Ikiwa una wakili, muombe wakili akupangie upya tarehe ya mahakama.